

CHUO CHA UKAMANDA NA UNAZIMU DULUTI-ARUSHA CHAZURU MANISPAA YA MOROGORO

Mkuu wa Chuo cha Ukamanda na Unazimu Duluti- Arusha, Brig. Gen. Steven Mnkande akiwa ameambatana na baadhi ya wakufunzi wa chuo hiko na wanafunzi, wamefanya ziara ya kimasomo katika Manispaa ya Morogoro ambapo wametembelea miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha kutoka Serikali Kuu na Mapato ya Ndani ya Manispaa.



Akiwa pamoja na timu yake katika eneo la ujenzi wa shule ya Sekondari Boma, inayojengwa kwa fedha za Mapato ya Ndani ya Manispaa, Brig.Gen. Mnkande amesema ukosefu wa elimu na ukosefu wa huduma bora za afya ni miongoni mwa viashiria vya ukosefu wa usalama wa mwanadamu, hivyo amempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dakta Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo hasa katika sekta za Elimu na Afya nchini ili kuhakikisha wananchi wanaelimika na kuwa na afya njema.



Kwa upande wao wanafunzi wa chuo hiko cha Ukamanda na Unazimu, wameushukuru uongozi wa Manispaa ya Morogoro kwa kuwapokea na kuhakikisha wanapata kile walicokuwa wamekusudia kukipata kupitia ziara yao.



Awali kabla ya Ziara hiyo, Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, ndugu Ally Machelo pamoja na Mkuu wa Divisheni ya Mipango na Uratibu wa Manispaa, ndugu Jeremiah Lubeleje walitoa historia fupi ya Manispaa ya Morogoro na namna ambavyo Manispaa inatekeleza miradi ya maendeleo ikiwa ni sehemu ya jitihada za kuhakikisha usalama wa raia kupitia Elimu, Afya na Uchumi.



Jumla ya wanafunzi 43 kutoka katika mataifa mbalimbali ikiwemo Zambia, Kongo, Kenya, Burundi, Rwanda, Uganda, Malawi na Tanzania wameshiriki katika ziara hii ambayo itadumu kwa muda wa siku saba ndani ya Mkoa wa Morogoro.



Mwisho